



Hapo zamani za kale,  
kulikuwa na kipindi kirefu  
cha kiangazi.  
Wanyamawalikula nyasi  
zote nchini. Kilichosalia  
pekee ni aina ya mmea  
uliotambaa kwenye miti  
mikubwa.



Siku moja Mbuzi alimwona  
Fisi akipita akiwa amekibeba  
kisu. Mbuzi alikiomba kile  
kisu ili aukate ule mmea  
uliotamba.



Fisi alimpa Mbuzi kisu.  
Mbuzi aliukata mmea ule  
akaula hadi akashiba kabisa.  
Alisahau kisu baada ya  
kukitumia.



Fisi alipokitaka kisu chake,  
Mbuzi hakujua afanyeje.  
Hakukumbuka alikokitupa.



Mbuzi alikwaruza hapa na pale akikitafuta kisu. Hadi leo, Mbuzi bado anakitafuta kisu hicho.



Fisi alimwambia Mbuzi,  
“Kwa sababu umekipoteza  
kisu changu  
kilichoniwezesha kupata  
riziki yangu, utakuwa mlo  
wangu. Vilevile nitawala  
wanao.”



Tangu siku hiyo, Fisi  
hajamhurumia Mbuzi.



Wakati huo huo, Mbuzi  
anaendelea kukitafuta kisu  
cha Fisi.